**KISWAHILI KIDATO CHA TATU**
**MUHULA WA TATU 2025**
**KARATASI YA PILI MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

Teacher.co.ke

***Majibu Ya Ufahamu***

(a) Yape makala haya kichwa mwafaka **(1x1)**
Wajibu wa kaunti/kazi ya kaunti

(b) Je? Kaunti inawajibikaje katika kuhudumia wananchi.
- i) Kutoa liuduma za afya kwa umma kama kujenga hospitali na vifaa vinavyotakikana
- ii) Kusimamia masuala ya uchukuzi pamoja na kukarabati barabara,
- iii) kuimarisha nyenzo za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi. ufugaji na ukuzaji wa Mimea.

**(3 x 1)**

(c) Utawala wa kaunti unaweza kupunguza vipi maafa yanayotokea kutokana na mapuuza ya mwanadamu
- i) kubuni sheria za barabarani pamoja na kukarabati
- ii) kutoa huduma muhimu za afya
- iii) kuimarisha usalama
- iv) kuthibiti matumizi ya dawa za kulevya

**(3 x 1)**

(d) Bunge la kitaifa lina wajibu gani katika serikali ya kaunti?
Kuunda sheria za kuzipa kaunti uwezo wa kuendeleza shughuli zake

(e) Ni changamoto zipi zinazoweza kukabili suala la ugatuzi nchini.
- i) Ufisadi
- ii) Uhaba wa fedha za kuendesha miradi ya maendeleo
- iii) Majukumu ya kaunti kuingiliwa na serikali kuu
- iv) Ukosefu wa wataalamu waliohitimu katika nyanja mbalimbali

**(3 x 1)**

f) Ni kwa njiani gani serikali ya kaunti inaweza kufufua uchumi wa nehi na kuinua kiwango cha maisha iii kufikia ruwaza ya 2030
- i) Kubuni nafasi za kazi
- ii) Kufufua na kuanzisha viwanda vya uzalishaji bidhaa
- iii) Kuimarisha miundo msingi

(g) (i) Uchukuzi - Kubeba mizigo na kusafirisha abiria
(ii) Ugatuzi - Ugavi wa mamlaka na rasilmali

**SEHEMU B: UFUPISHO**

2. (a) Sina lengo la kuzishambulia dini zetu na namuomba mungu asiniandikie dhambi.
   (b) Dini za uislamu na ukristo zinatuelekeza mwanamke kumheshimu mumewe na kumsikiliza anachosema.
   (b) Dini imewapa wanawake jukumu la kufuata amri ya mumeo.
   (c) Wanaume wengi wamechukua amri hii kunyanyasa na kuwanyima fursa ya elimu na hofu ya kupata kipato.
   (d) 90% ya wanawake hawatoi hoja kwa sababu wao wameiamini kuwa dini.
   (e) Wanaume huwa na hofu ya kupata changamoto kutoka kwa wake waliojiendeleza kielimu.
   (f) Dini zinaeleza umuhimu wa mtu kupata elimu bila kubagua.

   (Hoja – 6, Mtiririko 2, Jumla alama 8)

   (b)
   - Kwa kupata elimu.
   - Asikandamizwe kwa vyovyote.
   - Tutambue umuhimu wa mwanamke katika ujenzi wa taifa.
   - Atafute kipato cha familia.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

- Aweze kutoa maoni ya ujenzi wa nchi.
- Imani potovu za kidini zitupiliwe mbali.

(Mtiririko – 1 (alama 6)

**SEHEMU YA C:MATUMIZI YA LUGHA.(alama 25)**

a) i).e/i

ii)y/w

b) Chanagnua kwa kielelezo cha matawi.

Mayai viza yatatupwa jalani.

Sentensi sahili




***(8 x ½ = 4)***

c) Tungia maneno sentensi. (alama 3)

i) Kitenzi kishirikishi kipungufu.

Koome ni mtiifu.

t

ii) Nomino ya kikundi.

Mfano.Familia hii inapenda biashara.

iii) Kiwakilishji cha pekee cha –enye

-enye itumiwe kuonyesha dhana ya ‘kuwa na ‘/umilikaji.

Mf. Chenye maandishi kimepotea

iv) Kivumishi cha nomino.

Mf. Kijana mzee analala.

Askari polisi amefutwa kazi. ***(6× ½ =3)***

**Tanbihi**

Baada ya kutunga sentensi neno lengwa lipigwe mstari.

=Lazima

d) **Mfano**

Yohana atamjengea babake nyumba kwa matofali mwaka ujao.

i.Babake-SH.kitondo

ii.Nyumba-SH .kipozi.

iii.Matofali-SH.ala.

iv.Mwaka ujao-chagizo ya wakati. ***(4×1=4)***

e) Ukubwa

Jiji hili lina majitu/mijitu mengi mingi. ***(1×2=2)***

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

f) **Ukanushaji** **(alama 2)**

i) Mtoto asingeota ndoto,asingeamka.

ii) Mavitu asipofika rafikiye hataondoka.

***Au***

i) Mtoto hangetoa ndoto hangeamka.

ii) Kama mavitu hafiki,rafikiye hataondoka. ***(2×1=2)***

g)(i) Nazali ya kaakaa laini ng'

h) Juma alimtaliki Farida mwaka jana. ***(1×1=1)***

i.Mwalimu aliwamkua wanafunzi wake.

j. b) i) Ngeli ni kundi la nominoza aina moja

ii) Tunda – LI – YA

Kipepeo – A – WA

k) c) Babu alimchapa nyanya? (swali)

Babu alimchapa nyanya! (mshangao)

Babu alimchapa nyanya. (maelezo / taarifa)

l) ) si – kiwakilishi cha ukanushaji

ku – kiwakilishi cha wakatiuliopita

m – kiwakilisha cha mtendwa

karib – mzizi

ish – kiwakilishi cha kauli

a – kiishio

m) Nikienda – ki – ya masharti

Nitakipata – ki ya nafsi

Kile – ki ya ngeli

Kitoto – ki ya udogo (zozote 4 x ½)

n) Mtawasomea vitabu hivyo (2x1 = 2)

o) Jizi lile lilimkata mkono .

**4. ISIMUJAMII**

(a) (i) Lafudhini matamshi ya mzungmzaji yana yojitokeza kutokana na athari za lugha yake ya kwanza.

(ii) Pia ni upekee unajitokeza kwa mtu binafsi katika kuzungumza lugha ngeni. ( 1 x 2 = 2mks)

(iii) Athari ya lugha ya kwanza.

(iv) Athari ya lugha zinazomnguka mzungumaji.

(v) Maumbile katika ala za sauti. (2X1=2)

b) (i) Watu kutoelewana vyema wanapozungumza.

(ii) Huwa vugumu kupata ujumbe kamili kuhusu kinachozungumzwa.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes